# SHIRIKISHOSHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## KANUNI ZA SHIRIKISHO

TOLEO LA KWANZA

APRILI 2025

# YALIYOMO

UTANGULIZI ..... 4
1. KANUNI ZA USAJILI NA LESENI ZA WANACHAMA ..... 4
1.1. Usajili wa Wanachama: ..... 4
1.2. Leseni za Washiriki: ..... 4
1.3. Kupoteza na Kurudishwa kwa Uanachama: ..... 4
2. KANUNI ZA UCHAGUZI WA TBF ..... 4
2.1. Maandalizi ya Uchaguzi: ..... 4
2.2. Sifa za Wagombea: ..... 4
2.3. Mchakato wa Uchaguzi: ..... 5
3. KANUNI ZA NIDHAMU, MAADILI NA RUFAA ..... 5
3.1. Uvunjaji wa Maadili: ..... 5
3.2. Utaratibu wa Malalamiko: ..... 5
3.3. Kusikiliza Kesi: ..... 5
3.4. Adhabu zinazoweza kutolewa: ..... 5
3.5. Rufaa: ..... 5
3.6. Matumizi ya dawa za kulevya/kuongeza nguvu: ..... 5
3.7. Heshima kwa Waamuzi/Viongozi: ..... 5
3.8. Vifaa na Miundombinu: ..... 6
3.9. Mitandao ya Kijamii: ..... 6
4. KANUNI ZA UENDESHAJI WA KAMATI NA KAMISHENI ZA TBF ..... 6
4.1. Muundo: ..... 6
4.2. Majukumu: ..... 6
4.3. Maadili: ..... 6
5. KANUNI ZA UTATUZI WA MIGOGORO NA RUFAA ..... 6
5.1. Migogoro: ..... 6
5.2. Rufaa: ..... 6
6. KANUNI ZA KUDHIBITI MGONGANO WA MASLAHI ..... 6
6.1. Tamko la Migongano: ..... 6
6.2. Matumizi ya Rasilimali: ..... 7
6.3. Ufuatiliaji na Adhabu: ..... 7
7. KANUNI ZA MATANGAZO, UDHAMINI NA HAKI MILIKI ..... 7
7.1. Nembo na Bendera: ..... 7
7.2. Udhamini: ..... 7
7.3. Haki Miliki: ..... 7
8. KANUNI ZA FEDHA NA MATUMIZI YAKE ..... 7

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

8.1. Vyanzo vya Mapato ........ 7

8.2. Usimamizi wa Mapato ........ 7

8.3. Bajeti na Mipango ya Matumizi ........ 7

8.4. Utoaji wa Fedha ........ 8

8.5. Ukaguzi wa Hesabu ........ 8

8.6. Uwajibikaji na Uwazi ........ 8

9. MUONGOZO WA KANUNI NA MATUMIZI YAKE ........ 8

9.1. Muongozo ........ 8

9.2. Matumizi ........ 8

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

# UTANGULIZI

Miongozo huu wa nidhamu umeandaliwa kulingana na muongozo wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Duniani (FIBA) unaolenga kuhakikisha uwajibikaji na utawala bora ndani ya Dausho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) na kwa wadau wake wanaojihusisha na mchezo moja kwa moja kama wachezaji, makocha, waamuzi, viongozi, na wadau wote wa mpira wa kikapu kwa tabia zao na matendo yao.

NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA
... OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM

## 1. KANUNI ZA USAJILI NA LESENI ZA WANACHAMA

### 1.1. Usajili wa Wanachama:

Wanachama wote wapya wa TBF ni lazima waombe kupitia fomu maalum ya usajili inayotolewa na TBF. Fomu hiyo iambatane na nyaraka muhimu kama vile cheti cha usajili wa kikundi/klabu, orodha ya viongozi, na malipo ya ada ya usajili. Maombi hayo yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu ambaye atauwasilisha kwa Kamati ya Utendaji ndani ya siku 14 kwa uamuzi rasmi. Mwanachama atapokea barua rasmi ya kukubaliwa au kukataliwa.

### 1.2. Leseni za Washiriki:

Kila mshiriki wa shughuli za TBF (wakiwemo wachezaji, waamuzi, makocha, viongozi wa klabu au vyama) lazima awe na leseni hai inayotolewa na TBF. Leseni hizi zitahuishwa kila mwaka baada ya kulipa ada inayotangazwa na TBF. Hakuna atakayeruhusiwa kushiriki mashindano yoyote ya TBF bila leseni halali.

### 1.3. Kupoteza na Kurudishwa kwa Uanachama:

Mwanachama ambaye hatalipa ada za mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo atapoteza hadhi ya uanachama wake. Ili kurejeshwa, atatakiwa kulipa madeni yote, kuandika barua ya maombi, na kuidhinishwa na Kamati ya Utendaji.

## 2. KANUNI ZA UCHAGUZI WA TBF

### 2.1. Maandalizi ya Uchaguzi:

Kamati ya utendaji ya TBF itaanda taratibu zote za awali angalau siku 60 kabla ya uchaguzi kufanyika. Kamati hiyo itashirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), ambalo litatayarisha fomu za kugombea na taratibu zingine muhimu. Fomu zitatolewa mwezi mmoja kabla ya uchaguzi.

### 2.2. Sifa za Wagombea:

Kila mgombea wa nafasi yoyote ndani ya TBF lazima awe raia wa Tanzania, mwenye umri

usiopungua miaka 25, elimu ya angalau kidato cha nne, na uzoefu katika uongozi au shughuli za michezo. Kamati Maalum ya Uchunguzi wa Wagombea itahakikisha sifa hizi zinatekelezwa.

### 2.3. Mchakato wa Uchaguzi:

Uchaguzi utafanyika kwa njia ya kura ya siri ili kuhakikisha uhuru na haki. Baada ya kura kuhesabiwa, matokeo yatatangazwa rasmi, na viongozi walioteuliwa wataapishwa mbele ya wanachama kwa mujibu wa Katiba.

## 3. KANUNI ZA NIDHAMU, MAADILI NA RUFAA

OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

### 3.1. Uvunjaji wa Maadili:

Vitendo vya ubaguzi wa aina yoyote, rushwa, unyanyasaji, matumizi mabaya ya mitandao au rasilimali za TBF havikubaliki. Wadau wote wa TBF wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu.

### 3.2. Utaratibu wa Malalamiko:

Malalamiko yaandikwe kwa maandishi na kuwasilishwa kwa Kamati ya Nidhamu. Uchunguzi wa awali utafanyika ndani ya siku 7, na taarifa rasmi itawasilishwa kwa mtuhumiwa.

### 3.3. Kusikiliza Kesi:

Kamati ya Nidhamu itasikiliza kesi ndani ya siku 14 tangu kupokea malalamiko. Pande zote zitaruhusiwa kuwasilisha ushahidi na mashahidi wao.

### 3.4. Adhabu zinazoweza kutolewa:

Adhabu ni pamoja na onyo, kusimamishwa kwa muda, faini, au kufutiwa kabisa uanancha wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF).

### 3.5. Rufaa:

Rufaa dhidi ya uamuzi wa Kamati ya Nidhamu inaweza kukatwa ndani ya siku 7, na Kamati ya Rufaa italazimika kutoa uamuzi ndani ya siku 14.

### 3.6. Matumizi ya dawa za kulevya/kuongeza nguvu:

Mchezaji atakayekutwa na matumizi ya madawa ya kulevya au kuongeza nguvu, atafungiwa kwa muda au maisha kulingana na aina ya kosa.

### 3.7. Heshima kwa Waamuzi/Viongozi:

Wachezaji, viongozi, na mashabiki wanapaswa kuheshimu maamuzi ya waamuzi na viongozi wa mechi.

### 3.8. Vifaa na Miundombinu:

Uharibifu wa makusudi wa vifaa vya Shirikisho utachukuliwa kama kosa la kinidhamu na kifedha.

### 3.9. Mitandao ya Kijamii:

Mitandao itumike kwa uwajibikaji, kuepuka lugha ya matusi, uchochezi, au upotoshaji.

## 4. KANUNI ZA UENDESHAJI WA KAMATI NA KAMISHENI ZA TBF

### 4.1. Muundo:

Kila Kamati au Kamisheni ya TBF itaongozwa na Kamishna aliyeidhinishwa na Bodi, akisaidiwa na wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano.

### 4.2. Majukumu:

Kamati/Kamisheni itaandaa mpango kazi wa mwaka unaoainisha malengo, shughuli, bajeti, na vigezo vya utekelezaji. Ripoti ya utekelezaji iwasilishwe kila baada ya miezi mitatu.

### 4.3. Maadili:

Wajumbe wote wa kamati watasaini tamko la kutunza siri, kuepuka migongano ya maslahi, na kujiepusha na vitendo vya rushwa au upendeleo.

REGIST... OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## 5. KANUNI ZA UTATUZI WA MIGOGORO NA RUFAA

### 5.1. Migogoro:

Migogoro baina ya wanachama au viongozi itashughulikiwa kwanza kwa majadiliano ya ndani kupitia vyombo vya TBF. Kama hakuna muafaka, Kamati ya Usuluhishi itaingilia kati na kutoa mwongozo.

### 5.2. Rufaa:

Mhusika anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Kamati ya Usuluhishi ndani ya siku 14. Uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya TBF utakuwa wa mwisho.

## 6. KANUNI ZA KUDHIBITI MGONGANO WA MASLAHI

### 6.1. Tamko la Migongano:

Viongozi na watendaji wa TBF wanatakiwa kujaza fomu ya tamko la kutojihusisha na maslahi binafsi kila mwaka.

### 6.2. Matumizi ya Rasilimali:

Rasilimali za TBF, ikiwa ni pamoja na fedha, vifaa, majengo, au usafiri, hazitakiwi kutumika kwa manufaa binafsi bila idhini ya maandishi kutoka kwa Bodi.

### 6.3. Ufuatiliaji na Adhabu:

Wakaguzi na kamati husika zitahakikisha ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali. Ukiukaji wowote utapelekea hatua za kinidhamu au za kisheria.

## 7. KANUNI ZA MATANGAZO, UDHAMINI NA HAKI MILIKI

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM

### 7.1. Nembo na Bendera:

Nembo, bendera na majina ya TBF si mali ya mtu binafsi na matumizi yake yoyote nje ya TBF yanahitaji kibali cha maandishi kutoka kwa Kamati Tendaji.

### 7.2. Udhamini:

Mikataba yote ya udhamini lazima ipitiwe na kuidhinishwa na kamati tendaji ya TBF. Udhamini wowote usihatarishe heshima, maadili, au malengo ya TBF.

### 7.3. Haki Miliki:

Haki zote zinazohusiana na matangazo, picha, nembo, na mashindano ya TBF ni mali ya TBF. Watu binafsi au taasisi zitakazovunja haki hizi zitachukuliwa hatua za kisheria.

## 8. KANUNI ZA FEDHA NA MATUMIZI YAKE

### 8.1. Vyanzo vya Mapato

Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) litapata mapato yake kutoka kwa vyanzo mbalimbali kama ada za wanachama, udhamini, michango ya wahisani, mapato yatokanayo na mashindano, mauzo ya bidhaa zenye nembo ya TBF na vyanzo vingine halali vitakavyopitishwa na Bodi ya TBF.

### 8.2. Usimamizi wa Mapato

Mapato yote ya TBF yatalipwa kupitia akaunti rasmi ya benki ya TBF. Hakutakuwa na matumizi ya fedha taslimu bila idhini rasmi ya Raisi wa Shirikisho kwa kufuata utaratibu wa kifedha uliowekwa.

### 8.3. Bajeti na Mipango ya Matumizi

Kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha, TBF kupitia Kamati ya Utendaji itatayarisha

bajeti ya mwaka mzima. Bajeti hii itakaguliwa na kupitishwa na Bodi ya TBF. Kila Kamisheni ya TBF inapaswa kupanga matumizi yake kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.

### 8.4. Utoaji wa Fedha

Utoaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya shughuli za TBF utafanywa kwa kuzingatia mahitaji halali yaliyowasilishwa kwa maandishi. Maombi ya fedha lazima yaidhinishwe na Katibu Mkuu au Mweka Hazina kabla ya Raisi kutoa idhini ya fedha kutolewa.

### 8.5. Ukaguzi wa Hesabu

Hesabu za TBF zitakaguliwa kila mwaka na mkaguzi wa hesabu aliyesajiliwa. Ripoti ya ukaguzi itawasilishwa kwenye Bodi ya TBF na Mkutano Mkuu kwa ajili ya uthibitisho. Ukaguzi utafanyika kila mwaka ili kuhakikisha matumizi bora ya fedha na rasilimali zingine.

### 8.6. Uwajibikaji na Uwazi

Wafanyakazi wote wa TBF, makamishna na wahusika wa miradi wanawajibika kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha yanafanyika kwa uwazi, ufanisi na kwa kuzingatia taratibu za kifedha. Wale watakaobainika kutumia fedha za shirikisho vibaya watawajibishwa kisheria na kinidhamu.

## 9. MUONGOZO WA KANUNI NA MATUMIZI YAKE

### 9.1. Muongozo

Kanuni hizi zitatumika kulingana na uhitaji wake katika shughuli za kila siku za kuendeleza kikapu, Zitafanyiwa maboresho kila mwaka endapo kutatokea uhitaji kulingana na mabadiliko ya sharia za nchi, Sheria za uendeshaji Mchezo kutoka FIBA au ukosekanaji wa muongozo katika kanuni husika.

### 9.2. Matumizi

Kamati ya Utendaji ya Shirikisho itazingatia matumizi sahihi ya kanuni hizi kwa manufaa ya Mchezo na endapo kutatokea mgongano wa kanuni Kamati ya Utendaji itafanya maamuzi kulingana na uhitaji wa mazingira yaliyopo.

P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM

**Katibu Mkuu**
Mwenze Kabinda
Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF)

**Rais**
Michael Kadebe
Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF)